
# Kuzaliwa Na Mungu

Donald White



“NI BURE KAMA VILE BWANA ATOAVYO”

Kimechapishwa na

**Colonial Press**
Charlottesville, VA 22906

© Copyright 2008
by Colonial Baptist Church
Charlottesville, VA 22906

# KUZALIWA NA MUNGU

## Yaliyomo


| Sura | | Ukrasa |
|---|---|---|
| | Utangulizi | 2 |
| 1 | Mtu (Mwanadamu) Ana Mwili na Nafsi – Roho | 3 |
| 2 | Mwili wa Asili Ni wa Muda na Utapotea! | 4 |
| 3 | Nafsi ya Kiroho ni ya Milele na Itadumu Milele! | 5 |
| 4 | Ni Lazima Tutafakari Hali Ijayo ya Nafsi Zetu | 6 |
| 5 | Watu Wawili, Kuzaliwa Kuwili na Falme Mbili! | 8 |
| 6 | Kuzaliwa na Mungu Kuna Maana Gani? | 11 |
| 7 | Uwezo wa Kuwa mtoto wa Mungu Unatoka kwa Mungu | 12 |
| 8 | Aliyezaliwa kwa Mungu ana Hakikisho la Wokovu wa Milele | 14 |
| 9 | Waliozaliwa kwa Mungu Wameokolewa Milele! | 16 |
| 10 | Kuzaliwa kwa Mungu, ni Mabadiliko ya Ndani Mara! | 18 |
| 11 | Ulinzi wa Nafsi Sio Kibali Cha  Mwili Kutenda Dhambi | 19 |
| 12 | Dhambi za Mwilini na Dhambi ya Nafsini | 20 |
| 13 | Shetani Hutupiga vita Kupitia kwa Mwili | 22 |
| 14 | Mwili wako Hautakupa Mwelekeo wa Ujao wa Nafsi Yako | 23 |
| 15 | Tunaweza Kujua Tumezaliwa na Mungu! | 25 |
| 16 | Kufanya Uamuzi | 27 |
| 17 | Nifanyeje niwe Mtoto wa Mungu? | 29 |
| 18 | Majibu | 31 |

## ✿ Utangulizi ✿

***"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake; waliozaliwa, si kwa damu,*** *wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali* ***kwa Mungu"*** (1Yn 1:12-13).

Je, mtu aweza kuzaliwa na Mungu? Basi kuzaliwa na Mungu au "kuzaliwa mara ya pili" ni nini? Biblia hutwambia kuhusu Nikodemo, aliyemwuliza Yesu swali kuhusu kuzaliwa mara ya pili, "*Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee*?" (Yn 3:4). Nikodemo hakuwa mtu wa kawaida asiye na ufahamu. Kinyume na hivyo alikuwa kiongozi wa Wayahudi na, katika cheo hicho, alikuwa mwenye akili na aliyeelimika. Ila, Nikodemu hakuelewa Yesu alipomwambia, "*Amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi kuuona ufalme wa Mungu*" (Yn 3:3).

Swali hilo lililoulizwa na Nilodemu linaulizwa na watu wengi wenye nia njema, wanaotafuta kweli. Huzuni ni kwamba, ni watu wachache tu ambao wamechukua muda wa kuyachunguza maandiko wapate ufafanuzi wa kuzaliwa kiroho. Wengi wanaojaribu kufafanua tendo hili la ajabu wameadhiriwa na mitindo yenye uzushi ya tamaduni za kanisa au maoni ya watu, bila kufuata Ukweli Wa Biblia. Hebu tuzingatie ujumbe huu muhimu wa Biblia: **Kuzaliwa kwa Mungu**.

Katika fundisho lolote, kutafuta ukweli kunahitaji kuwa jambo kuu, lakini lazima tukubali ya kwamba ukweli umewekwa na Mungu, sio mwanadamu. Katika somo hili tutazingatia ukweli wa Biblia tukizingatia utu wa nje, mwili na utu wa ndani, nafsi (roho) ya mwanadamu. Mwanadamu yuko na mwili na roho.

## 1. Sura ya Kwanza

## Mtu (Mwanadamu) Ana mwili na Nafsi – Roho

### 🕮 <u>Somo la Biblia</u>:

Mathayo 10:28, "*Msiwaogope wauuao* ***mwili****, wasiweze kuiua na* ***roho****; afadhali mwogopeni yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika Jehanum*."

1 Wakorintho 15:44b, "*Ikiwa uko mwili wa asili na wa roho pia uko*."

2 Wakorintho 4:16, "*Kwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku*."

1 Petro 2:11, "*Wapenzi, nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na* ***roho***."

Mathayo 26:41, "*Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni! Roho I radhi, lakini mwili ni dhaifu*."

### ☞ <u>Tamati</u>:

Biblia inafundisha wazi kuwa mwanadamu ana:

(1) Utu wa nje, mwili, **na**
(2) Utu wa ndani, roho (nafsi)

### ✍ <u>Maswali</u>:

1. Kuna mwili wa __________ na kuna mwili wa __________.
2. Utu wa nje ni _____________ na utu wa ndani ni ________.
3. Mwili wa asili pia huitwa utu wa _____________ na roho pia huitwa utu wa ________________.
4. Tunahitaji kumwogopa Mungu yule anaweza kuangamiza _____________ na _____________ katika Jehanum.

## 2. Sura ya Pili

## Mwili wa asili Haudumu na Utaharibiwa.

---

### 🕮 **Somo la Biblia:**

Waebrania 9:27a, "*Na kama vile watu wanavyo wekewa kufa mara moja…*"

Warumi 5:12, "*Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi.*"

Warumi 7:18a, "*Kwa maana uajua ya kuwa ndani yangu (yaani ndani ya mwili wangu) halikai neno jema.*"

Warumi 7:24, "*Ole wangu, maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?*"

1 Petro 1:24, "*Maana mwili wote ni kama majani, Nafahari yake yote ni kama ua la majani.Majani hukauka na ua lake huanguka.*"

Mwanzo 3:19, "*Kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa: kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.*"

1 Wakorintho 15:50, "*Ndugu zangu, nisemayo ni haya, ya kuwa nyama na damu haziwezi kuurithi ufalme wa Mungu; wala uharibifu kurithi kutokuharibika*"

### ☞ **Tamati:**

Mwili wetu wa asili hauna ahadi ya kuishi milele, hauna wokovu wa milele na matumaini ya milele. Utakufa na kupotea.

### ✍ **Maswali ya kujifunza:**

1. Mwili wa asili hauwezi kuishi milele; ni lazima ___________.
2. ___________ ikawafikia watu wote kwasababu wote wamefanya dhambi.
3. Bibilia yatufunza ya kwamba, mwili wa asili ulitoka _______________ na utarudi ______________.
4. ________ na _______ haziwezi kuurithi ufalme wa Mungu.
5. Hakuna _____________ ya kuishi milele kwa mwili wa asili.

## 3. Sura ya Tatu

## Nafsi ya Kiroho ni ya Milele na Itadumu Milele!

---

📖 **<u>Somo la Biblia</u>:**

Daniel 12:2, "*Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele.*"

Mathayo 25:34, "*Kisha mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, **Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu**.*"

Mathayo 25:41, "*Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake.*"

Mathayo25:46, "*Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele.*"

Matendo ya Mitume 24:15b, "***ya kwamba kutakuwa na ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio haki pia.***"

1 Yohana 2:25, "*Na hii ndiyo ahadi aliyotuahidi, yaani, uzima wa milele.*"

2 Wathesalonike 1:7b-9, "*Wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu ...katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasiotii injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele...*"

☞ **<u>Tamati</u>:**

Wakati nafsi ya kiroho (Mtu wa ndani) itatenganishwa na mwili wa asili (Mtu wa nje), hiyo nafsi itakuwa milele, na ufahamu wa kuishi huenda mbinguni au Jehanamu.

✍ **<u>Maswali ya kujifunza</u>:**

1. Mtu wa ndani (au nafsi) ataishi __________________.
2. Nafsi nyingine zitakuwa na uzima wa ____________ na nyingine zitakuwa na kudharauliwa ___________________.
3. Wasioamini wataishi katika ____________ wa milele na katika ________________ ya millele.
4. Mungu alihaidi uzima wa _____________ kwa wale waliompokea Yesu Ksristo kama Mwokozi.

## 4. Sura ya Nne

## Ni Lazima Tutafakari hali Ijayo ya Nafsi Zetu

### Utangulizi:

Kwa kawaida, watu wengi hupanga ujao wao wa mwili na kupuuza ya kwamba Mungu yuko na hali ya ujao wa nafsi zao za milele. Mtu wa namna hii ni mpumbavu kabisa.
Zaburi 14:1, "***Mpumbavu amesema moyoni, Hakuna Mungu****…*"
Mwanadamu anafanya mipango mikubwa katika maisha yake na anakazana kufanikisha maisha yake: kujiburudisha, kuonekana, elimu, afya, kazi, fedha na kustaafu. Nguvu nyingi zinatumika kutunza mwili ambao uko leo na kesho unarudi mavumbini. Ila, hatujihusishi kuwaza ambako nafsi itakaa milele. Katika mtazamo wa vifungu vifuatavyo, inaonekana ni bora kujitayarisha kukutanana Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu.

### Somo la Biblia:

Kumbukumbu la Torati 32:29, "*Laiti wangekuwa na akili, hata wakafahamu haya,* ***ili watafakari mwisho wao****.*"

*Mhubiri 11:8,* "*Naam, mtu akiishi miaka mingi, na aifurahie yote, lakini* ***na azikumbuke siku zijazo za giza****, kwa maan zitakuwa nyingi…*"

Yeremia 29:13, "*Nanyi* ***mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote****.*"

Amosi 4:12b, "*na kwa sababu nitakutenda hivi,* ***ujiweke tayari tayari kuonana na Mungu wako, Ee Israeli****.*"

Yohana 3:3b, "***Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuona ufalme wa Mungu****.*"

Yohana 3:18, "*Amwaminiye yeye hahukuiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.*"

Matendo ya Mitume 16:31, "*...Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako.*"

Warumi 14:11-12, "*... kama niishivyo, anena Bwana, kila goti litapigwa mbele zangu; na kila ulimi utamkiri Mungu. Basi ni hivyo, kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu.*"

2 Petro 3:7, "*Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto, kwa neno lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu.*"

☞ **<u>Tamati</u>:**

Kuna maswali ambayo sis sote tunahitaji kujiuliza. Ni wapi nafsi yangu itakaa milele? Jemoyo wangu ni wa Mungu? Je, mimi niko tayari kusimama mbele ya Mungu na nihukumiwe kwa dhambi zangu? Kuzeeka na kudhoofika kwa mwili na ufupisho wa maisha. Sisi sote tutasimama mbele ya Mungu hivi punde kuliko jinsi tunavyofikiria. Yesu alipeana mwelekeo mwepesi kwa mtu wa ndani kukutana na Mungu. Yesu alisema, "***Hamna budi kuzaliwa mara ya pili***" (Yohana 3:7b).

✍ **<u>Maswali ya kujifunza</u>:**

1. Yapasa watu wote ________ _____________ kukutana na Mungu mwenye nguvu.
2. Tunampata Mungu wakati tunamw____________ yeye kwa moyo wetu wote.
3. Ni _______________ asemaye hakuna Mungu.
4. Wale ambao wanamw____________ hawatahukumiwa, lakini wale wasiomw_______________ wameshahukumiwa tayari.
5. Kila mtu miongoni mwetu atatoa ___________ mbele za Mungu.

## 5. Sura ya Tano

## Watu Wawili, Kuzaliwa Kuwili na Falme Mbili!

### ☝ Utangulizi:

Kuelewa neno, "**kuzaliwa na Mungu**," ni lazima tulinganishe kati ya yale ambayo ni ya kimwili na yale ambayo ni ya kiroho. Yesu hudhihirisha tofauti hii kati ya mtu ambaye ni wa mwilini na wa kiroho (mwili na nafsi), kuzaliwa halisi na kuzaliwa kiroho (kuzaliwa na kuzaliwa mara ya pili, na ufalme wa kimwili na ufalme wa kiroho (ufalme wa ulimwengu huu na ufalme wa Mungu). Somo letu linaturudisha nyuma kwa Nikodemo, mkuu wa Wayahudi, akamjia Yesu kupewa mawaidha (Yohana 3:1-8). Nikodemo alimtambua Yesu alikuwa mwalimu kutoka kwa Mungu na hii huenda ni kwa sababu ya miujiza aliyoifanya.

### 🕮 Somo la Biblia:

Yohana 3:3, "*Yesu akajibu, akamwambia Amini, amini, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.*"- Tafadhali, tia makini maneno "*mara ya pili"* wakati Yesu alisema, "kuzaliwa mara ya pili," neno, "mara ya pili" linatuelekeza kwa kuzaliwa kwa awali.

Yohana 3:4, "*Nikodemo akamwambia, Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa?*"

Nikodemo hakuelewa ukweli wa kiroho alioilezwa na Yesu. Alifikiria kuhusu kuzaliwa kimwili na akajua ni vigumu kuzaliwa kimwili mara ya pili. Ni hakika kuwa Nikodemo hakuweza kutafautisha kati ya mwilini na ya kiroho kwa hivyo, hangeweza kuelewa.

Yohana 3:5, "*Yesu akajibu, Amini, amini nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu...*" Kiini cha mstari ni huu, "Mtu asipozali wa *kwa maji na kwa Roho...*" Waalimu wengine wa Bibilia huamini ya kuwa, "*maji*" katika Yohana 3:5 inaonyesha Roho Mtakatifu au Maji ya Neno la Mungu. Waalimu wengine huamini ya kuwa Yesu aliendelea kuelezea hali sambamba za kuzaliwa kimwili na kuzaliwa kiroho kwa kumsaidia Nikodemo afahamu kwa urahisi ukweli wa kuzaliwa mara ya pili. Hata ikiwa Yesu alitumia kuzaliwa kimwili kueleza kuzaliwa kiroho, ninaamini, ufafanuzi wa "kuzaliwa kwa maji" kunalingana pia na yale maji ya uzazi. Waalimu wa Bibilia wanakubaliana kuwa maandishi haya hayaelezi kabisa kuhusu ubatizo, kama tafsiri ya "maji" katika Yohana 3:5. Haya maji yanadhihirisha, kuzaliwa, sio kufa, *bali* ubatizo unapeana picha au mfano wa kufa, kuzikwa na kufufuka, sio kuzaliwa:

> "… *kwa njia ya ubatizo katika mauti yake*?" (Warumi 6:3)
>
> "*Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo …*" (Wakolosai 2:12)

Ubatizo wa maji ni kitendo (kazi) cha mwilini, na hakiwezi kuokoa, bali ni picha ya Injili ya Yesu Kristo. Kifo, kuzikwa na kufufuka kwake (1 Wakorintho 15:1-4).

Mwandishi anaamini "maji" katika Yohana 3:5 inamaanisha maji ya uzazi;

inatilia uzito wazo la aina mbili za kuzaliwa. Akinamama hukumbuka matukio ya kuwazaa watoto wao: **maji hutoka**!! Maji huwa ni dalili ya kuwa mtoto atazaliwa katika ufalme wa dunia hii (kuzaliwa kimwili) na inadhihirisha vyema vile Roho Mtakatifu humleta mwamini katika ufalme wa Mungu (kuzaliwa kiroho).

Yohana 3:6, "*Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni Roho.*" --Tena, Yesu akatofautisha kati ya kuzaliwa kwa mwili na kuzaliwa kwa kiroho. Kama mtu amezaliwa na mzazi, huyo aliyezaliwa ni wa mwili. Tena, kile kilichozaliwa kwa roho ni roho. Mbegu inazaa kwa jinzi yake. Kuzaliwa kwetu kwa kwanza ni kutoka kwa mbegu ya baba wetu wa dunia (ya mwili na iharibikayo). Kuzaliwa kwa mara ya pili ni kutoka kwa mbegu ya Baba wetu wa Mbinguni (ya roho na isiyoharibika). Vifungu vya Yohana 3:6 na 1 Petro 1:23 zote zaonyesha kuzaliwa kwa kwanza (mwilini) na kuzaliwa kwa pili (roho) ambako ni kwa Mungu. 1 Petro 1:23, "*Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele*."

Hebu sasa tutumie jedwali hii kuelezea zaidi.

| **Kuzaliwa** | **Kuzaliwa mara ya pili** |
|---|---|
| Kuzaliwa kwa mbegu iharibikayo ya mwilini | Kuzaliwa kwa mbegu isiyoharibika ya Mungu |
| Kuzaliwa kwa hali ya asili | Kuzaliwa kwa roho |

Yohana 3:7, "*Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, Hamna budi kuzaliwa mara ya pili.*" Bwana wetu anatumia "mara ya pili," akionyesha kuzaliwa kwa kiroho.

Yohana 3:8, "*Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho*" -- "aliyezaliwa kwa Roho" inaonyesha Roho Mtakatifu au "**kuzaliwa na Mungu.**"

Tunaweza kuona mafundisho ya Yesu kwa Nikodemo (Yohana 3:1-8) kwa kuendelea kutumia jedwali hii:

| **Ya Asili** | **Ya Kiroho** |
|---|---|
| Ufalme wa ulimwengu huu | Ufalme wa Mungu |
| Kuzaliwa kwa mwili | Kuzaliwa kwa Roho |
| Kuzaliwa kwa kwanza | Kuzaliwa kwa pili |
| Kuzaliwa (mfano) - kif. 3 | Kuzaliwa tena |
| Kuzaliwa kwa maji - kif. 5 | Kuzaliwa kwa roho (Mungu) |
| Kuzaliwa kwa mwili - kif. 6 | Kuzaliwa kwa roho (Mungu) |
| Kuzaliwa (mfano ) - kif. 7 | Kuzaliwa tena. |

Mkazo wa kuzaliwa na Mungu (kuzaliwa kwa pili) kunarahisishwa na vifungu vifuatavyo:

Yohana 1:12-13, "*Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika* ***watoto wa Mungu****, ndio wale waliaminio jina lake,* ***waliozaliwa*** *si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu*."

Tunaweza, kulingana na Neno la Mungu, kufanyika wana wa Mungu. Huu ni uhusiano wa kiroho pamoja na mtu wa kiroho. Uhusiano huu huongezeka kutokana na imani katika Yesu Kristo sio kwa kudai kwa gharama. Mtu hawezi kuingia katika familia ya Mungu kwa matendo ya dini, kutenda mema, pesa, ubatizo, ushirika wa kanisa, au kitu kingine cha "mwilini." Kuzaliwa Upya ni kwa kiroho. Tunazaliwa na Mungu (mwanzo mpya) tunapotubu, tunageuka kutoka kutokuamini kwetu na kwa imani tunampokea Yesu Kristo kama Mwokozi.

Wacha tutumie jarida kwa Yohana 1:13, kuonyesha mwili na nafsi.

| **Mwili wa Asili**<br>(kuzaliwa kwa mwili) | **Mwili wa Roho**<br>(Kuzaliwa kwa roho) |
|---|---|
| Kuzaliwa kwa damu - kif 13 | Kuzaliwa si kwa damu |
| Kuzaliwa kwa mapenzi ya mwili | Kuzaliwa si kwa mapenzi ya wili |
| Kuzaliwa kwa mapenzi ya mwanadamu | Kuzaliwa si kwa mapenzi ya mwanadamu |
| Kuzaliwa kwa mwili | Kuzaliwa kwa Mungu |

Bibilia inaeleza wazi tofauti kati ya wale ambao mwanzo wao (kuzaliwa) ni kwa wazazi wa ulimwengu, na wale pia ambao mwanzo wao (kuzaliwa) kwa Mungu. Ni mtu wa ndani ambaye ni wa kiroho aweza kuzaliwa kwa Mungu na apate maisha ya milele na Mungu.

## ☞ Tamati:

Neno la Mungu linafundisha wazi umuhimu wa "**kuzaliwa na Mungu.**" Iwapo mtu hajapata **kuzaliwa kwa pili** (kuzaliwa na Mungu), Mtu wa pili (nafsi) hataona au kuingia katika ufalme wa pili (Ufalme wa Mungu).

## ✍ Maswali ya kujifunza:

1. Yesu akasema, "Mtu asipozaliwa ________ ____ ________ hawezi kuona ufalme wa Mungu."
2. Kuzaliwa kwa kwanza ni kuzaliwa kwa ___________ na kuzaliwa kwa pili ni kuzaliwa kwa _____________.
3. Tunapozaliwa kwa roho, tunakuwa wana au watoto wa ______________.
4. Kuna watu wawili: Mtu wa _______________ Na mtu wa _________________.
5. Kuna kuzaliwa kuwili: Kuzaliwa kwanza kwa _____________ au kuzaliwa kwa pili kwa __________________.
6. Kuna falme mbili: Ufalme wa huu wa ______________ na ufalme wa ___________________.

## 6. Sura ya Sita

## Kuzaliwa na Mungu Kuna Maana Gani?

### ☝ Utangulizi:

Kuzaliwa kunaama ya kuibuka, hali ya kuwa hai, au kugeuka., Ufafanuzi wa kwaida ni **Mwanzo**. Hii huelezea mwanzo wa maisha, mbali nje ya tumbo la mama, ndiyo kwa tamadani zetu siku yetu ya kuzaliwa.

### 🕮 Somo la Biblia:

Yesu amwambia Nikodemo: "*Amini, amini nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuona ufalme wa Mungu*" (Yohana 3:3b).

Yesu alieleza kwamba, kwa Nikodemu kuuona ufalme wa Mungu, ni lazima azaliwe katika ulimwengu wa roho, kama alivyozaliwa katika ulimwengu wa mwili. Tunaweza kusema, ni lazima tuwe na mabadiliko ya mwili ili kuwa wa familia ya dunia hii na lazima tuwe na mabadiliko yo kiroho ili kuwa wa familia ya Mungu.

### ☞ Tamati:

"*Kuzaliwa mara ya pili*" ni mwanzo mpya, au maisha mapya ndani ya Kristo, ambayo inafanyika wakati tunaamini Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, kutubu dhambi zetu na kumpokea yeye kama Bwana na Mwokozi. Mwanzo mpya ni **kuzaliwa na Mungu!**

### ✍ Maswali ya kujifunza:

1. Maana rahisi inayotumiwa kwa kuzaliwa mara ya pili ni kuwa na ____________________ mpya.
2. Yesu alieleza Nikodemo ya kwamba kuzaliwa kwake kwa mwili au mwanzo wake wa maisha haukutosha. Ni lazima azaliwe ________ ___ ________ .
3. Ili kuzaliwa mara ya pili, Nikodemo lazima awe na mwanzo mpya au kuzaliwa kupya kwa __________________ .

## 7. Sura ya Saba

## Uwezo wa Kuwa Mtoto wa Mungu Unatoka kwa Mungu

---

### ☝ Utangulizi:

Yohana 1:12, "*Bali wote waliompokea aliwapa uweza wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake,*" Mwanandamu hawezi kupata wokovu kwa uwezo wake mwenyewe, nguvu au mali, bali anaweza kupokea kama zawadi. Watu wengine wanaamini kuwa, wanastahili kuwa wana wa Mungu kwa sababu ya wema wao, haki au ushirika wa dini. Watu kama hao wanatazamia akili zao na nguvu zao za kimwili, bila kutambua ya kwamba wokovu kipawa kutoka kwa Kristo.

Warumi 10:3, "*Kwa maana, wakiwa hawaijui haki ya Mungu, na wakitaka kuithibitisha haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki ya Mungu.*"

### 🕮 Somo la Biblia:

**Sababu tatu kwa nini Mungu pekee anapeana wokovu**:

(1) Mtu wa asili hawezi kufanya kitu, kuleta maisha mapya kwa mtu wa ndani. Mwili uko chini ya hali ya asili.

Warumi 7:18a, "*Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu, yaani, ndani ya mwili wangu halikai neno jema;*"

Warumi 3:23, "*Kwa Sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.*"

Warumi 6:23, "*Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.*"

Waefeso 2:8-9, "*Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu.*"

(2) Mtu wa asili hawezi kufahamu mambo ya kiroho.

1 Wakorintho 2:14, "*Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni.*"

Ni jambo la kushangaza kuwa baadhi ya watu werevu ulimwenguni hawawezi kushika ukweli wa mambo ya kiroho. Nikodemo hangeweza kufahamu na alikuwa ni mkuu. Siku hizi, wengi hawafahamu.

Marko 10:15, "*Amini, nawaambieni, yeyote asiyeukubali ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hatauingia kabisa.*"

Tabia ya nafsi ya mwanadamu hukataa imani kama ya mtoto.

Waefeso 4:17-19, "*...tangu sasa msienende kama mataifa waenendavyo, katika ubatili wa nia zao; ambao; akili zao zimetiwa giza, nao wamefarikishwa na uzima wa Mungu, Kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao, ambao wakiisha kufa ganzi wanajitoa katika mambo ya ufisadi wapate kufanyiza kila namna ya uchafu kwa kutamani.*"

2 Timotheo 2:7, "*Yafahamu sana hayo nisemayo, kwa maana Bwana atakupa akili katika mambo yote.*"

(3) Wokovu hupeanwa tu kama kipawa. Huustahili kuupata au kununua. Tunaweza kupata karama hii kwa imani.

Yohana 3:16, "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*"

Yohana 4:10, "*Yesu…Akamwambia, kama ungalijua karama ya Mungu, naye ni nani akwambiaye, Nipe maji ninywe ungalimwambia yeye, naye angalikupa maji yaliyo hai.*"

Warumi 6:23b, "*...bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Ksristo Yesu Bwana wetu.*"

2 Wakorintho 9:15, "*Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo.*"

Waefeso 2:8, "*Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu.*"

## ☞ **Tamati:**

Wokovu unapokelewa kwa masharti ya Mungu sio masharti yetu. Wokovu sio kitu tunachodai, bali ni kipawa ambacho Yesu Ksristo huwapa waamini. Kwa imani tunampokea Yesu Kristo, tunakubali karama ya Mungu ya wokovu wa milele na kufanyika watoto wa Mungu. *Yohana 1:12,* "*Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake.*"

## ✍ **Maswali ya kujifunza:**

1. Uwezo wa kufanyika mtoto wa Mungu unatoka kwa _________ .
2. ____________ kitu mtu wa asili anaweza kufanya kudai au kununua wokovu wa mtu wa ndani (roho).
3. Mtu wa asili hawezi kufahamu mambo ya ___________ ___ ______________.
4. Wokovu ni _____________ kutoka kwa Mungu na hauwezi kudaiwa au kununuliwa.

## 8. Sura ya Nane

## Aliyezaliwa kwa Mungu ana Hakikisho la Wokovu wa Milele.

---

☝ **Utangulizi:**

Watu wengi wana dini ya mwili, na wachache wana wokovu wa nafsi. Ni bure kutafuta hakikisho la wokovu, kama mtu hajapata wokovu. Hakuna wokovu kwa matendo mema, dini au makanisani; ni imani pekee ndani ya Yesu Kristo huleta wokovu na hakikisho kamili.

🕮 **Somo la Biblia:**

Yohana 3:14-16, "*Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye. Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee. Ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*"

Yohana 3:36, "*Amwaminiye mwana yuna uzima wa milele." Asiyemwamini mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia.*"

**Milele ni kudumu na kuendelea!** Hii ni ahadi ya Mungu, ambaye hawezi kusema uongo. Maisha ya milele ni maisha ambayo hayana mwisho. Maisha yoyote ambayo yana mwisho si (na haijawahi kuwa) maisha ya milele. **Hakuna kumbukumbu ndani ya Bibilia ya kuonyesha kuwa mtu yeyote amewahi kuokolewa mara mbili.** Tunapata kipawa cha Mungu cha uzima wa milele mara moja na kinadumu milele.

Waefeso 4:30, "*Wala msimhuzunishe yule Roho mtakatifu wa Mungu; ambaye mlitiwa* ***muhuri*** *hata siku ya ukombozi.*" –Hili neno, "Muhuri," linamaanisha kuimarisha au kudhibitisha kikamilifu. Sisi ni wake Mungu.

2 Timotheo 1:12b, "*Kwa maana namjua yeye niliyemwamini, na kusadiki ya kwamba aweza* ***kukilinda*** *kile nilichokiweka amana kwake hata siku ile.*" Mungu ana uwezo kabisa wa, "kulinda" nafsi ya milele.

Warumi 8:31, "*Basi tuseme nini juu ya hayo?* ***Mungu akiwa upande wetu ni nani aliye juu yetu?***"

Warumi 8:35a, "***Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo?***"

Warumi 3:38-39, "*Kwa mana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala wenye mamlaka , wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.*"

Warumi 10:9, "*Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.*"

Yohana 10:27-29, "Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata. Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu. Baba yangu aliyenipa hao ni mkuu kuliko wote; wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya

katika mkono wa Baba yangu."

Waebrania 10:14, " *Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.*"

2 Timotheo 4:18, "*Bwana ataniokoa na kila neno baya, na kunihifadhi hata nifike ufalme wake wa mbinguni. Utukufu una yeye milele na milele Amina.*"

1 Petro 1:3-5, "*Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu; tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu. Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho.*"

Kama waamini, sis ni:

- ☑ **Tumeokolewa**
- ☑ **Tumetiwa muhuri**
- ☑ **Tumehifadhiwa**
- ☑ **Tumetakaswa**
- ☑ **Tumelindwa**

Kwa uwezo wa Mungu Mwenyezi, na Yesu Kristo anaombea wale walio wake. Sisi pia tuna hakikisho la kutosha la wokovu wa milele, kujua Muumba wa ulimwengu (Yohana 1:3) anatuombea. Anatuombea kwa Baba yake na wao ni moja. (Yohana 10:30).

Yohana 17:9, "*Mimi nawaombea hao; siombei ulimwengu; bali hao ulionipa, kwa kuwa hao ni wako*."

Waebrania 7:25, "*Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee*."

Kuwa na hakikisho kamili la wokovu, ni lazima tufahamu na kulenga hitaji. Yesu Kristo alikuja kuokoa **nafsi** ya mwanadamu, si mwili wake. Paul alisema katika 2 Timotheo 2:7, "*Yafahamuni sana hayo nisemayo, kwa maana Bwana atakupa akili katika mambo yote.*"

## ☞ Tamati:

Iwapo tunaamini Mungu na Bibilia kuwa kweli, nilazima pia tuamini nafsi ambayo "imezaliwa kwa Mungu," **imeokolewa**, **imetiwa mhuri, imehifadhiwa, imetakaswa**, **na kulindwa milele na Mungu**. Kwa mwamini, hii ni hakikisho la wokovu.

## ✍ Maswali ya kujifunza:

1. Mtu hawezi kuandaliwa wokovu ikiwa hawezi __________wokovu.
2. Waamini wame ________ hadi siku ya ukombozi.
3. Mungu ana nguvu ya kuzi ______nafsi zetu tunapoielekeza kwake.
4. Yesu alisema, atatupatia uzima wa milele kwa waumini na hawata ________________.
5. Wale waliotakaswa ______________ milele.
6. Mtume Paulo alisema, Bwana atam __________ hata afike ufalme wa mbinguni.

## 9. Sura ya Tisa

## Waliozaliwa kwa Mungu Wameokolewa Milele!

---

### 🕮 <u>Somo la Biblia</u>:

Warumi 4:8, "*Heri mtu yule ambaye Bwana hamhesabii dhambi.*"
1 Yohana 3:6, "*Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi: kila atendaye dhambi hakumwamini yeye, wala hakumtambua.*"
1 Yohana 3:9, "*Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu.*"
1 Yohana 5:4-5, "*Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huishinda ulimwengu, na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu. Mwenye kuushinda ulimwengu ni nani isipokuwa ni yeye aaminiye ya kwamba Yesu ni mwana wa Mungu.*"
1 Yohana 5:18, "*Twajua yakuwa kuwa kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; bali yeye aliyezaliwa na Mungu hujilinda wala yule muovu hamgusi.*"

Ufunguo kwa kwa mstari wa juu ni "**kila aliyezaliwa kwa Mungu.**" Kwa sababu ya kuchanganyikiwa na kushindwa kufahamu Neno la Mungu, Wengi wa waalimu wa Bibilia hufunza maana ya "*usitende dhambi*" kama: "*usiendelee kufanya dhambi.*" Dosari katika fundisho hili ni "matendo" inalenga mwili wa asili ila mistari iliyo hapa juu inalenga mwili wa kiroho. Tena, tunaona ukosefu wa kutofautisha kati ya mwili na roho.
Je maneno "**kila aliyezaliwa kwa Mungu**" yanalenga mwili (mtu wa nje) au roho (mtu wa ndani)? Je ni mwili wa nje uliozaliwa kwa Mungu? La hasha! Mwili si wa mbegu ya Mungu, wala mtu wa nje kuzaliwa au mzaliwa wa Mungu. Mwili umezaliwa kwa mbegu ya kuharibika una hali ya dhambi; shauku ya dhambi na tamaa, na hupiga vita dhidi ya roho. Mistari iliyopo hapo juu haidhihirishi kutokuwa na dhambi kwa mtu wa nje wa asili. Asili, hali ya mwili (mtu wa nje) kila mara ni mazoea ya kutenda dhambi mradi tu kuna uzima katika mwili. "**Kila aliyezaliwa kwa Mungu**" ni hali ya ndani, nafsi ya rohoni.
1 Yohana 5:1a, "***Kila mtu aaminiye kwamba Yesu ni Kristo amezaliwa na Mungu:***" Ni mtu wa ndani ambaye huamini au kutoamini. Kutoamini (dhambi ya mtu wa nje) ni dhambi ya pekee ambayo huleta hukumu ya milele kwa nafsi. Dhambi ya mwili huleta uharibifu na mauti. *(Wagalatia 6:8; Waebrania 9:27).*
Yohana 3:18, "*Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu*."

### ☞ <u>Tamati</u>:

"***Yeyote ambaye amezaliwa kwa Mungu hawezi kutenda dhambi***"
Ni nafsi ya roho ndani ya mtu ambayo imezaliwa na Mungu haina na haiwezi

kutenda dhambi. Dhambi ambayo inalemea nafsi ni kutoamini! Imani huondoa kutokuamini na nafsi huwekwa huru. Yeyote aliyezaliwa na Mungu, na hawezi kutenda dhambi, hiyo nafsi imeokolewa milele na haiwezi kupotea au kuhukumiwa Jehenamu. *Waebrania 10:14,* "*Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.*"

## ✍ **Maswali ya kujifunza:**

1. "Kila mtu aliyezaliwa kwa Mungu" inalenga mtu wa _____________ na sio mtu wa ________________ .
2. Kila mtu aaminiye Yesu ni Kristo ni ame__________ ___ ___________ .
3. "Tunajua ya kwamba kila mtu aliyezaliwa na Mungu ____________________ ______________."
4. "Kila aliyezaliwa na Mungu hatendi ____________________."
5. Kama nafsi haiwezi kutenda dhambi, nafsi hiyo itahukumiwa au ipotee milele? ❑ Ndio ❑ La

## 10. Sura ya Kumi

## Kuzaliwa Kwa Mungu, ni Mabadiliko ya Ndani Mara!

☝ **Utangulizi:**

Mabadiliko halisi na ya mara hufanyika mara kwa mtu wa ndani (kiroho) wakati mtu anampokea Kristo. Hata hivyo, pamoja na mabadiliko haya ya ndani vinatokea vita kati ya mwili wa asili wa zamani na hali ya mpya wa kiroho.

🕮 **Somo la Biblia:**

2 Wakorintho 5:17, "*Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya*."

Wagalatia 6:15, "*Kwa sababu kutahiriwa si kitu, wala kutokutahiriwa bali kiumbe kipya*."

Warumi 7:23, "*Lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali* ***inapiga vita na ile sheria ya akili zangu****,…*"

Warumi 8:7-9, "*Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu. Kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kutii, Wala waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu. Lakini ikiwa roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamuifuati mwili, bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake*."

1 Petro 2:11, "*Wapenzi, nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho*."

☞ **Tamati:**

"Kiumbe kipya" ni mtu wa ndani mwenye ubadilisho wa nia, mwenendo na hali ya roho. Kama matokeo ya ubadilisho huu, hali mpya ya roho na hali ya zamani ya mwili inaubishi wa kuthibiti mwili. Kama tunavyo kuwa karibu na Kristo au Imara katika imani, tunakuwa na nguvu kushinda na kuthibiti hali ya mwili na tabia ya mwili.

✍ **Maswali ya kujifunza:**

1. Wale ambao wamezaliwa kwa Mlungu ni ________________ wapya.
2. Kwa wale walio ndani mwa Kristo ___ ___________ yamepita na mambo yote yamekuwa ________________.
3. Sheria ya viungo vya mwili hupigana ______________ na hali ya roho ya wale ambao wamezaliwa kwa Mungu.
4. Ile nia ya mwili ni uadui na _________________.

## 11. Sura ya Kumi na Moja

# Ulinzi Wa Nafsi Sio Kibali Cha Mwili Kutenda Dhambi

☝ **Utangulizi:**

Wakristo hakika wengine husizitiza eti mafundisho ya ulinzi wa uzima wetu wa milele ni kibali cha kuishi kama ibilisi na bado wanaenda mbinguni. Tena, kuchanganyikiwa kuhusu mwili (mtu wa nje) na nafsi (mtu wa ndani) kunasababisha dosari. *Warumi 6:1-2*, "*Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?*"

🕮 **Somo la Biblia:**

Warumi 7:22-25, "*Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa wa ndani, lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili zangu, na kuifanya mateka ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu. Ole wangu, maskini mimi! Ni nani atakeyeniokoa na mwili huu wa mauti? Namshukuru Mungu, kwa Yesu Kristo Bwana wetu, Basi, kama ni hivyo, mimi mwenyewe kwa akili zangu naitumikia sheria ya Mungu, bali kwa mwili wangu sheria ya dhambi.*"

Warumi 8:1, "*Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, Wale ambao hawatembei kwa mwili bali kwa roho.*"

1 Petro 2:11b, "*...Ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho.*"

☞ **Tamati:**

Mtu wa ndani ambaye amezaliwa kwa Mungu ni kiumbe kipya na hana shauku ya kutimiza tamaa za mwili, bali anakazana kuzishinda na kuthibiti shauku na tamaa za mwili, na huhuzunika wakati mwili unaposhinda. Mtu ambaye hali yake ya kiroho hupenda kutosheleza dhambi za mwili, yeye si kiumbe kipya na hajawahi kuzaliwa kwa Mungu!

✍ **Maswali ya kujifunza:**

1. Hali ya mwilini hupiga ______________ kupigana na hali mpya.
2. Hatustahili kuendelea na dhambi za mwili kuijaribu ___________ ya Mungu.
3. Kama waaminio, tu______ ___________ tamaa za mwili.
4. Waaminio, wasitembee, si kwa ______________, bali kwa _____________ .

## 12. Sura ya Kumi na Mbili

## Dhambi za Mwilini na Dhambi ya Nafsini

---

### ☝ Utangulizi:

Unaweza kuuliza, "Kuna dhambi tofauti za mwili wa asili na mwili wa kiroho?" Ndio, natilia mkazo ndio! Ingawa tuna makanisa ambayo hufundisha ya kwamba wokovu ni ukamilifu bila dhambi wa mwili wa asili, hiyo haiwezekani wala sio kulingana na Bilbia. Mwenendo wa Mkristo huonekana kwa mtu wa nje, au maisha, lakini tambua kuwa mwili wa asili au mtu wa nje huwa na vita na mtu wa ndani kila mara. Mkristo, baada ya kuweka tumaini lake kwa Yesu Kristo, huwa kiumbe kipya, na hali mpya ya mtu wa ndani. Mkristo anavyo endelea kukomaa, hujikaza kuweka hali ya mwili wa asili chini katika kiasi na utiivu. Bibilia inashughulikia yote mawili: mwili wa asili na ule wa kiroho, lakini wengi, huenda kwa kupenda au kutojua, huonekana hawana ufahamu wa hali ya kiroho. Ni jambo la "asili" kwetu sote kukazia yanayoonekana ila ni "ya kiroho" ni kwa wale waliozaliwa na Mungu kuangalia yale ya kiroho.

Maandiko yafuatayo yanaonyesha tofauti hasa ya kipekee.

### 🕮 Somo la Biblia:

(1) Maandiko yasema sote hutenda dhambi!

Warumi 3:9-10, "*Ni nini basi? Tu bora kuliko wengine? La! Hata kidogo. Kwa maana tumekwisha kuwashitaki Wayahudi na Wayunani ya kwamba pia wamekuwa chini ya dhambi; kama ilivyoandikwa, ya kwamba, hakuna mwenye haki hata mmoja.*"

Warumi 3:23, "*Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.*"

1 Yohana 1:8-10, "*Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe wala kweli haimo mwetu. Tukiziungama dhambi zetu,Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. Tukisema kwamba hatukutenda dhambi, twamfanya yeye kuwa mwongo wala neno lake halimo mwetu.*"

(2) Maandiko yanasema waliozaliwa kwa Mungu hawatendi dhambi. .

1 Yohana 3:6, "*Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi, kila atendaye dhambi hukumwona yeye, wala hakumtambua.*"

1 Yohana 3:9, "*Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi, kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu.*"

1 Yohana 5:4a, "***Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu***;"

1 Yohana 5:18, "***Twajua ya kuwa kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi;*** *bali yeye aliyezaliwa na Mungu hujilinda, wala yule mwovu hamgusi.*"

## ☞ **Tamati:**

Katika pointi (1) na (2), hapo juu, huenda ikawa kinyume cha Neno la Mungu, kama mtume Yohana hakuwa akibainisha kati ya mtu wa asili na mtu wa kiroho.

Pointi ya (1) inaeleza kuhusu dhambi za nje, katika mwili wa asili; na

Pointi ya (2) inaeleza kuhusu hali ya kutokuwa na dhambi kwa mtu wa kiroho wa ndani, kwa wale waliozaliwa na Mungu.

## ✍ **Maswali ya kujifunza:**

1. "______________ wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."
2. "Tukisema kwamba ________________ dhambi, twajidanganya wenyewe."
3. Mungu _________________ dhambi yule anayeamini (Warumi 4:8).
4. Dhambi moja inayohukumu nafsi ni ile ya ______________ (angalia sura ya tisa).

## 13. Sura ya Kumi na Tatu

## Shetani Hutupiga vita Kupitia kwa Mwili

☝ **Utangulizi:**

Kulingana na 1 Yohana 2:16, dhambi zote za mwili zinaweza kugawanywa katika maeneo matatu.: 1. *Tamaa ya mwili*; 2. *Tamaa ya macho*; 3. *Kiburi cha maisha.*

🕮 **Somo la Biblia:**

Hebu sisi tumfahamu Hawa katika bustani ya Edeni. Hawa alikuwa na makosa katika maeneo yote matatu alipoamua kula tunda lililokatazwa (Mwanzo 3:6):

1. Matunda yalikuwa yafaa kwa chakula (tamaa ya mwili).
2. Yalipendeza macho (tamaa ya macho).
3. Ulitamanika kwa kupeana maarifa (Kiburi cha uzima).

Hawa alikuwa na hatia ya dhambi hizi za mwilini, lakini kabla ya kushindwa na majaribu yale ya kimwili, Hawa alikuwa na hatia ya dhambi kubwa ya ndani ya kiroho. Dhambi ya kwanza ya Hawa ilikuwa katika mtu wake wa ndani. Hawa hakuamini na kuweka matumaini yake kwa Mungu na Neno lake!

Maeneo haya matatu, huhusika na dhambi zote za mwilini, ikiwemo Daudi (2 Samweli 11:2-6) na Samson (Waamuzi 14:1-12). Tunaona katika Mathayo 4:1-10 jinsi Shetani alijaribu Bwana wetu katika maeneo haya matatu. Shetani alimshawishi Yesu kwa:

1. Kushibisha **mwili** kwa kuamuru mawe yawe mkate, mstari wa, v. 3.
2. Kushibisha **macho** kwa kuangalia ufalme wote wa ulimwengu, v.8.
3. Kushibisha **kiburi cha uzima** kwa kudhibitisha yeye ni mwana wa Mungu, v.6.

☞ **Tamati:**

Mwokozi wetu alikuwa mshindi juu ya mwili. Alikuwa mkamilifu na asiye na dhambi kama mwanadamu na Mungu. Wagalatia 5:24, "*Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulibisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake.*" Wakristo ni lazima wasulubishe na kuudhibiti mwili kama wanataka kuwa washindi katika ulimwengu huu.

✍ **Maswali ya kujifunza:**

Shetani anapigana na kila mmoja kupitia maeneo ya msingi ya mwili wa dhambi.

1. Tamaa ya __________.
2. Tamaa ya __________.
3. ___________ cha uzima.

## 14. Sura ya Kumi na Nne

## Mwili wako Hautakupa Mwelekeo wa Ujao wa Nafsi Yako

---

### ☝ <u>Utangulizi</u>:

Wengine huamini watu wema wanaenda mbinguni, na watu wabaya wanaenda kuzimuni. **Hii sio ukweli!** Kama ni watu wema tu huenda mbinguni, hakuna yeyote ambaye angelikuwa huko kwa sababu, "*Hakuna mtenda mema, La! Hata mmoja*" *(Warumi 3:12b).* Kama ni watu wabaya tu huenda kuzimu, sisi sote tungelikuwa huko kwa sababu, "*Wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu*" *(Warumi 3:23).* Sote tufahamu kuwa wengine walioenda Jehenamu, na mmoja aliyenda mbinguni na tofauti.

### 🕮 <u>Somo la Biblia</u>:

**<u>Mtu tajiri</u>**: Luka 16:22- 23, "*Yule tajiri naye akafa, akazikwa, Basi, kule kuzimu aliyainua macho yake, alipokuwa katika mateso…*" Biblia haitatupa habari za mtu huyu wala maovu yake ingawa watu wote ni watenda dhambi. Yule tajiri alimwuliza Baba Ibrahimu amtume Lazaro awashuhudie ndugu zake, "*wasije wale pia wakafika mahali hapa pa mateso*" (v. 28c). Ibrahimu akamwambia, "*wasipowasikia Musa, na manabii, hawatashawishwa hata mtu akifufuka katika wafu*" (v. 31). Ni hakika kuwa tajiri hakuamini Mungu alipokuwa duniani, bali aliamini alipokuwa kuzimu. Aliamini, lakini alikuwa amechelewa!

**<u>Yule Farisayo</u>**: Luka 18:11-14 inaelezea maisha ya Farisayo. Alishuhudia kuwa yeye hakuwa mnyang'anyi, mdhalimu, mzinzi, hufunga mara mbili kwa juma, hutoa zaka katika mapato yake yote, na alikuwa kawaida kiongozi wa dini. Alitegemea wema wake yeye mwenyewe kuliko kutegemea Yesu Kristo. Yesu alisema wazi kwamba Farisayo yule hakuhesabiwa haki.

**<u>Mfalme Agripa</u>**: Wakati mtume Paulo alikuwa akimwambia mfalme Agripa, alisema, "*Mfalme Agripa, Je! Wawaamini manabii? Agripa akamwambia Paulo, kwa maneno machache karibu unifanye mimi kuwa Mkristo*" (Matendo ya Mitume 26:27-28). Mfalme Agripa alikuwa na mamlaka juu ya hekalu la Yerusalemu na alikuwa ndiye anamtawaza kuhani mkuu. Bibilia haijapeana habari yoyote kuonyesha kuwa mfalme Agripa alikuwa mwovu, lakini ni wazi alikufa bila Yesu.

**<u>Mwizi Msalabani</u>:** kumbuka mwizi aliyekuwa juu ya msalaba pamoja na Yesu? Alikiri ya kwamba alihukumiwa haki na alikuwa anastahili adhabu ya kifo. Hatuna habari yoyote kuonyesha ya kwamba mwizi huyu alitenda wema hata moja, Kijiunga kwa kanisa, kutoa zaka, au kubatizwa. Mtu huyu hakuwa mwema, lakini alimwamini Yesu. Hii inaonyeshwa kwa kuungama dhambi, kukubali Yesu kuwa ni Bwana, na ombi lake kwa Yesu. Yesu alimwambia mtu huyo Muovu, "*Leo hivi utakuwa pamoja nami peponi.*" (Luka 23:43b).

## ☞ **Tamati**:

- ☑ Hakuna dhambi ya mwilini imewahi kuituma nafsi kwa adhabu ya milele.
- ☑ Hakuna wema wowote wa mwili umewahi kuiingiza nafsi moja mbinguni.
- ☑ Dhambi ambayo inaangamiza nafsi milele ni ile ya KUTOAMINI.
- ☑ Wokovu wa milele wa nafsi ni kipawa cha Mungu kwa WANAOAMINI.
- ☑ KUAMINI na KUTOAMINI ni matendo ya mtu wa ndani, sio ya mwilini, na yeyote ambaye ANAYEMTUMAINI Yesu Kristo hatakuwa na sababu ya KUTOAMINI. Mtu wa ndani (nafsi), ambaye amezaliwa na Mungu, hawezi kutoamini (dhambi) na nafsi hiyo haiwezi kupotea.

Kama hii inaonekana ngumu, tafadhali tazama: 1 Yohana 3:6, 5:4 na 5:18.

## ✍ **Maswali ya kujifunza**:

1. Watu ambao wanajikaza kuwa wema (machoni pa ulimwengu) wanaweza kwenda Jehanamu milele? ❑ Ndio ❑ La
2. Je wale ambao wanajulikana kuwa waovu kisha wakubali kuzaliwa na Mungu wanaweza kupokea ahadi ya mbinguni? ❑ Ndio ❑ La
3. Dhambi ya ____________________ ni dhambi moja ambayo inahukumu nafsi kwenye adhabu ya milele.

## 15. Sura ya Kumi na Tano

## Tunaweza Kujua Tumezaliwa na Mungu!

☝ **Utangulizi:**

Watu wengi hufikiria wamezaliwa na Mungu kwa sababu ya matendo yao mema au maisha yao ya kidini badala ya kumwamini na kumtegemea Yesu. Wakristo wengi wa dhati wamejisalimisha wenyewe kwa Bwana, lakini hawana hakika kwamba wamezaliwa na Mungu. Ujuzi haba ya Biblia unaleta shaka. Tunapokuwa na shaka, tunastahili kufanya uchunguzi. Mambo yafuatayo manne yatasaidia kuangalia na kuuchunguza wokovu wako.

🕮 **Somo la Biblia:**

☑ Angalia matunda yako.

Kwa sababu ya kuwa kiumbe kipya, mwamini wa kweli atatamani kuuthibiti mwili. Mkristo mpya anapoendelea kukomaa, anapata uwezo wa kuuthibiti mwili wake zaidi na anazaa matunda.

Yohana 15:5, "*Mimi ni Mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana…*"

Mathayo 7:15-16, "*Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali. Mtawatambua kwa matunda yao…*"

Mathayo 7:20, "*Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua*."

Waebrania 6:8, "*Bali ikitoa miiba na magugu hukataliwa na kuwa karibu na laana; ambayo mwisho wake ni kuteketezwa*."

☑ Angalia unaporudiwa na Mungu kwa dhambi

Wakati Wakristo wanashindwa kuwa na kiasi mwilini, Mungu huwashughulikia kama Baba anayejali watoto wake wasiotii. Mungu huwarudi walio wake.

Waebrania 12:6-8, "*Maana yeye ambaye Bwana ampenda, humrudi, Naye humpiga kila mwana amkubaliye. Ni kwa ajili ya kurudiwa mwastahimili; Mungu awatendea kama wana; maana ni mwana yupi asiyerudiwa na babaye? Basi kama mkiwa hamna kurudiwa, ambako ni fungu la wote, ndipo mmekuwa wana wa haramu ninyi, wala si wana wa halali*."

☑ Angalia uwepo wa Roho Mtakatifu wa Mungu ndani ya maisha yako.

1 Wakorintho 3:16, "*Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu*?"

Warumi 8:14, "*Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu*."

Warumi 8:16, "*Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu*."

☑ Angalia Neno la Mungu

1 Yohana 5:13, "*Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu*."

2 Timotheo 2:15, "*Jitahidini kijionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali Neno la kweli*."

2 Timotheo 3:16-17, "***Kila andiko lenye pumzi ya Mungu****, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema*."

## ✍ **Maswali ya kujifunza**:

1. Kama tunakaa ndani ya Kristo (ya mzabibu) tutazaa ______________ mengi.
2. Kama tumezaliwa na Mungu na hatuna kiasi kuhusu tamaa zetu, tuta__________ na Mungu.
3. Roho Mtakatifu wa Mungu anashuhudia pamoja na roho za waamini kwamba wao ni __________________ na Mungu.
4. Kusudi mojawapo la kusoma na kujifunza neno la Mungu ni ili tujue ya kuwa tuko na ___________ ____ ____________ .

## 16. Sura ya Kumi na Sita

## Kufanya Uamuzi

### ☝ Utangulizi

Yoshua 24:15b, "... *Chagueni hivi leo mtakayemtumikia…*"
Roho Mtakatifu wa Mungu humletea kila mmoja wetu mahali katika maisha yetu ambako tunamtambua Mungu na maisha ya milele ni hakika; ndipo ni lazima tufanye uamuzi ya tutakavyofanya kuhusu uhusiano wetu na Mungu.

Ni vigumu kuvunja itikadi za zamani, mitindo ya dini na mashaka, lakini yeyote yule aweza tu kumpokea Yesu Kristo kwa imani. Uamuzi ulio mkuu zaidi ni kuamua maisha yetu ni milele - **kuwa au kutokuwa na Yesu Kristo kama Mwokozi.**

Ni uamuzi wa kweli wa **maisha ya milele** au **mauti ya milele**. Tunapojifunza Neno la Mungu, tunaona kuwa dhambi huleta mauti na wote hufa kwa sababu ya dhambi. Kwa wote wasioamini kutakuwako na mauti ya nafsi zao, ambayo ni kutenganishwa milele kutoka kwa Mungu na adhabu ya milele kuzimu.

### 🕮 Somo la Biblia:

☑ Maandiko yafuatayo yanaonyesha kuwa dhambi huleta mauti:

Warumi 6:23, "*Kwa **maana mshahara wa dhambi ni mauti**, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.*"

Mwanzo 2:17, "*Walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika,*"

Warumi 5:12, "*Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti, na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi.*"

Ezekieli 18:4c, 20a, "***Roho ile itendayo dhambi itakufa.***"

Ufunuo wa Yohana 20:14-15, "*Mauti na kuzimu zitatupwa katika lile ziwa la moto. Na iwapo mtu yeyote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.*" Mstari huu unagusia kuhusu adhabu na hali ya kutisha ya milele ya nafsi. Kama tunaangalia dhambi ya asili ambayo ilileta mauti ya asili kwa mwili, au dhambi ya kiroho ambayo inaleta mauti ya nafsi. Mungu anasema "*mshahara wa dhambi ni mauti.*"

☑ Shukuru Mungu kuna uchaguzi mwingine, ni **UZIMA**!

Yohana 3:14-16, "*Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye. Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipootee, bali **awe na uzima wa milele**.*"

Yohana 17:3, "*Na **uzima wa milele ndio huu**, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.*"

Wagalatia 6:8, "*Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu, bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho* ***atavuna uzima wa milele***."

☞ **Tamati:**

**Ni** uamuzi **wetu:**

**Uzima au Mauti;**
**Mbingu au Kuzimu;**
**Yesu Kristo au Shetani!**

Yohana 3:17-18, "*Maana Mungu hakumutuma Mwana ulimwenguni ili ahukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika Yeye. Amwamuniye Yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.*"

✍ **Maswali ya kujifunza:**

1. Ni lazima tuchague leo _______________ ___________.
2. Nafsi itendayo dhambi ita____________ .
3. Wale wanaomwamini YesuKristo watapata __________ ___ ____________ .
4. Chaguo letu ni:
   Uzima au ____________ .
   Mbingu au ______________.
   Yesu Kristo au ________________.

## 17. Sura ya Kumi na Saba

## Nifanyeje niwe Mtoto wa Mungu?

---

### 🕮 <u>Somo la Biblia</u>:

Yohana 3:15-16, "*Ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye. Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*"

Yohana 5:24, "*Amin, amin, nawaambia, yeye alisikiaye Neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani.*"

Yohana 11:25, "*Yesu akamwambia, mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi.*"

Yohana 12:46, "*Mimi nimekuja ili niwe nuru ya ulimwengu, ili kila mtu aniaminiye mimi asikae gizani.*"

Yohana 20:31, "*Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini muwe na uzima kwa jina lake.*"

Matendo ya Mitume 16:30-31, "*...Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka? Wakamwambia, mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka…*"

Warumi 10:9, "*Kwa sababu, ukimkri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa, Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.*"

1 Yohana 5:la, "***Kila mtu aaminiye kwamba Yesu ni Kristo amezaliwa na Mungu****…*"

Mithali 3:5, "***Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote****; wala usizitegemee akili zako mwenyewe.*"

### ☞ <u>Tamati</u>:

Tuna hakikisho ya kutosha tunaweza kuokoka. Tunaweza kuwa watoto wa Mungu. Tunaweza kumiliki uzima wa milele. Lile ambalo ni lazima tufanye, kulingana na Neno la Mungu, ni kumwamini Yesu Kristo. Hii haimaanishi tu kuamini kumhusu Yesu, au kuamini kuwa Yesu alikuwa shujaa wa historia: hata mashetani huamini. "*Wewe wamini ya kuwa Mungu ni mmoja; watenda vema. Mashetani nao waamini na kutetemeka*." (Yakobo 2:19).

Kufanyika mwana wa Mungu, **Ni lazima tuamini kwa kiwango cha kumtegemea!** Kuamini kwa kweli ni kumkubali Yesu kama Mwokozi wa nafsi yetu ya milele, kutubu dhambi zetu na kumtii Yeye milele. Tunaweza, kwa imani, kufanya uchaguzi wa kumkubali Yesu kama Bwana wa maisha yetu na Mwokozi wa nafsi zetu milele. Sasa: "*…tazama, wakati uliokubalika ndio sasa; tazama siku ya wokovu ndiyo sasa.*" (2 Wakorintho 6:2b)

Mungu anakupenda, na kwa vile umesoma hadi kufikia hapa, wewe huenda unajali uhusiano wako na Mungu. Je! Unaweza sasa hivi kumwitia Bwana kwa moyo wako?

## ✝ Ombi

**Ee Mungu, Ninakuja kwako katika jina la Yesu Kristo. Ninaamini kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, ya kwamba alikufa pale msalabani Calvari kwa ajili yangu, na kwamba yeye ni Kristo aliyefufuka. Mimi sasa hivi, nampokea Yesu Kristo kuwa Mwokozi wangu na ninahidi kumtii, kumtumikia na kuwa ushuhuda kwa wengine kwa upendo na neema yake. Ninakushukuru kwa kunipenda mimi na kwa karama yako ya wokovu ambayo ninapokea katika jina la Yesu. Amen.**

## ✍ Maswali ya kujifunza:

1. _______________ Bwana kwa moyo wako wote, wala usizitegemee __________ zako mwenyewe.
2. " _____________ Bwana Yesu Kristo nawe utaokoka."
3. "Kila anaye _____________ kwamba Yesu ni ______________ amezaliwa na Mungu."
4. Swali la mwisho na la maana kabisa ni: Umekwisha au utaweka imani yako na matumaini kwa Yesu Kristo?
   ❑ Ndio ❑ La

## 18. Sura ya Kumi na Nane

## Majibu

**Sura ya kwanza 1**
1. Nyama, nafsi (1 Wak. 15:44)
2. Nyama, nafsi
3. Nje, ndani (2 Wak. 4:16)
4. Nafsi, mwili (Mat. 10:28)

**Sura ya Pili 2**
1. Kufa (Ebr 9: 27)
2. Mauti (War 5:12)
3. Mavumbini, mavumbini (Mwa. 3:19)
4. Nyama, Damu (1 Wak. 15:50)
5. Tumaini

**Sura ya 3**
1. Milele (Mat. 25:46)
2. Milele, milele (Dan 12:2)
3. Moto, adhabu (Mat 25:41, 46)
4. Uzima (Mat. 25:46; 1 Yohana 2:25)

**Sura ya 4**
1. Kuwa tayari (Amosi 4:12)
2. Tafuta (Yer. 29:13)
3. Mpumbavu (Zaburi 14:1)
4. Amin, Amin (Yohana 3:18)
5. Hesabu (War. 14:12)

**Sura ya 5**
1. Mara ya pili (Yohana 3:3)
2. Mwili, nafsi (Yohana 3:6)
3. Mungu (Yohana 1:12-13)
4. Nje, ndani (1 Wak. 15:44)
5. Mwili, kiroho (Yohana 3:6
6. Ulimwengu, Mungu (2 Wak. 4:4, Yohaha 3:3)

**Sura ya 6**
1. Mwanzo
2. Mara ya pili (Yohana 3:3)
3. Nafsi (Yohana 3:6)

**Sura ya 7**
1. Mungu (Yohana 1:12)
2. Hakuna (War. 3:23, Wae. 2:8-9)
3. Hali ya roho (1 Wak. 2:14, Mar. 10:15)
4. Karama (War. 6:23)

**Sura ya 8**
1. Kumiliki
2. Tiwa muhuri (Wae. 4:30)
3. Weka (2 Tim. 1:12)
4. angamia (Yohana 10:27-30)
5. Amewakamilisha (Wae. 10:14)
6. hifadhi (2 Tim. 4:18)

**Sura ya 9**
1. Ndani, nje (1 Yohana 3:9)
2. Zaliwa na Mungu (1 Yohana 5:1)
3. Hatendi dhambi (1 Yohana 5:18)
4. Dhambi (1 Yohana 3:9)
5. La

**Sura ya 10**
1. Viumbe (2 Wak. 5:17)
2. Vya kale, mpya (2 Wak. 5:17)
3. Vita (War. 7:23)
4. Mungu (War. 8:7-9)

**Sura ya 11**
1. Vita (War. 7:22-25)
2. Neema (War. 6:1-2)
3. Weke mbali (1 Petro 2:11)
4. Mwili, roho (War. 8:1)

**Sura ya 12**
1. Wote (War. 3:23)
2. Hatuna (1Yohana 1:8)
3. Hamhesabii (War. 4:8)
4. Kutoamini (Yohana 3:18)

**Sura ya 13**
1. Mwili (1Yohana 2:16)
2. Macho (1 Yohana 2:16)
3. Kiburi (1 Yohana 2:16)

**Sura ya 14**
1. Ndio (Tazama Luka 18:11-14)
2. Ndio (Tazama Luka 16:22-23 na Luka 23:43)
3. Kutoamini (Yohana 3:18)

**Sura ya 15**
1. Matunda (Yohana 15:5)
2. Rudiwa (Wae 12:6-8)
3. Watoto (War 8:16)
4. Uzima wa milele (1 Yohana 5:13, 2 Tim. 2:15)

**Sura ya 16**
1. Tutamtumikia Bwana (Yoshua 24:15)
2. Kufa (Eze. 18:4)
3. Uzima wa (Yohana 3:14-16)
4. Mauti, kuzimu, Shetani

**Sura ya 17**
1. Mtumaini, akili (Mithali 3:5)
2. Aamini (Matendo ya Mitume 16:31)
3. Aamini, Kristo (1 Yohana 5:1)
4. Ndio